JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

Menejimenti ya Utumishi wa Umma,
S.L.P. 2483,
Dar es Salaam,
Tanzania.

Kumb. Na. C/AC 45/257/01/60

15 Aprili, 2004

WARAKA WA UTUMISHI WA UMMA NA. 1 WA MWAKA 2004 KUHUSU UTEKELEZAJI WA SHERIA YA UTUMISHI WA UMMA, 2002 (SHERIA NA. 8 YA 2002)

1.0 UTANGULIZI

Kutokanana Serikali kutunga Sheria ya Utumishi wa Umma Na 8 ya mwaka 2002 na Kanuni za Utumishi wa Umma 2003, Waraka huu unatolewa kama mwongozo wa utekelezaji wa Sheria na Kanuni ambayo ndio chimbuko la utaratibu mpya wa uwajibikaji na usimamizi wa utumishi wa umma. Mambo ya msingi ya Sheria na Kanuni hizi ni kuonyesha mwelekeo wa utendaji kazi katika utumishi wa umma kwa kuzingatia malengo na matokeo (performance management) na mikataba ya kazi (performance contracts), na usimamizi thabiti wa watumishi wa Umma.

2.0 MABADILIKO YA MSINGI:

2.1 Kuundwa kwa Utumishi wa Umma:

Serikali imeunda utumishi wa umma mmoja ambao umeunganisha makundi mbalimbali yafuatayo:-

(a) Utumishi wa Serikali Kuu;
(b) Utumishi wa Serikali za Mitaa; (c) Utumishi wa Afya;
(d) Utumishi wa Ualimu;
(e) Utumishi waHuduma za Zimamoto na Uokoaji na Utumishi wa Uhamiaji;
(f) Utumishi wa Wakala wa Serikali na Taasisi za Serikali.

2.2 Kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi wa Umma

Sheria imeanzisha Tume ya Utumishi wa Umma (PUBLIC SERVICE COMMISSION) ambayo kwa sasa ina Idara tano kulingana na makundi ya utumishi yaliyotajwa hapa juu. Tume hii ndiyo inayohakikisha kuwa utumishi wa umma ni mmoja na kuwa watumishi wote wana taratibu za usimamizi, hadhi, haki na maslahi yanayofanana. Hivyo, kazi kubwa ya Tume ya Utumishi wa Umma ni kuhakikisha kuwa masuala ya utumishi yanaendeshwa kwa haki na usawa na yanalenga katika utendaji wenye malengo maalum.

2.3 Usimamizi wa Kazi

Viongozi na Watendaji sehemu za kazi ndio wasimamizi wakazi na watakuwa mamlaka ya ajira, upandishaji vyeo na Kusimamia nidhamu ili kuimarisha uwajibikaji.

Ili kuleta utendaji mzuri, mikataba ya utendaji (performance contracts) itatumika, na watumishi wote watasaini mikataba hiyo na wasimamizi wao wa kazi.

3.0 MAMLAKA ZA AJIRA NA NIDHAMU

Utaratibu wa Usimamizi, Ajira na Nidhamu katika Utumishi wa Umma utakuwa kama ifuatavyo:-

- **Rais:**
  Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Rais ndiye msimamizi mkuu wa Utumishi wa Umma. Ndiye mwenye mamlaka ya juu kabisa katika utumishi wa umma na watumishi wote wanatekeleza majukumu yao kwa niaba ya Rais. Rais ndiye mamlaka ya uteuzi ya Viongozi Wakuu Serikalini.
- **Katibu Mkuu Kiongozi:**
  Ndiye Mkuu wa Utumishi wa Umma. Anatoa dira ya uongozi na sura ya utumishi wa umma. Anahakikisha kuwa ndani ya Utumishi wa Umma kuna uwajibikaji na utendaji unaozingatia matokeo ya kazi na huduma bora inayoridhisha. Pia yeye ni mamlaka ya kuwathibitisha kazini na ya nidhamu kwa watumishi wanaoteuliwa na Rais. Vile vile ni mamlaka ya nidhamu ya watumishi wote wa umma pale ambapo ataona inafaa kuchukua hatua

za kinidhamu. Hivyo ni mamlaka ya juu ya kiutawala katika kutoa masharti ya utendaji kazi katika utumishi wa umma.

- **Waziri mwenye dhamana ya Utumishi wa Umma:**
  Sheria, hususan Kifungu Na.34 (1), inampa mamlaka ya kutunga Kanuni za Utumishi wa Umma (Public Service Regulations). Kanuni za Utumishi wa Umma 2003 ndizo zinazotoa mwongozo wa utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma, kuhusiana na taratibu mbalimbali za ajira na usimamizi katika Utumishi wa Umma. Kadhalika ndiye mwenye mamlaka ya kutunga Taratibu za uendeshaji wa utumishi wa umma (Public Service Scheme): Taratibu za Uendeshaji wa Utumishi wa Umma za 2003, zilizotungwa chini ya Kifungu 7(1) cha Sheria, ndizo zinatoa maelekezo ~ ya matumizi ya madaraka na mamlaka kama ilivyofafanuliwa kwenye Sheria, Kanuni, maagizo na maelekezo ya Serikali yaliyopo na yatakayyokuwa yakitolewa mara kwa mara.

- **Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa:**
  Ni mamlaka ya ajira na nidhamu ya Wakurugenzi wa Halmashauri isipokuwa wale wa Majiji na Tume ambao huteuliwa na Rais.

- **Makatibu Wakuu, Wakuu wa Idara Zinazojitegemea na Makatibu Tawala wa Mikoa, Kamishna wa Huduma za Zimamoto na Uokoaji, Mkurugenzi wa Uhamiaji, Wakurugenzi wa Halmashauri za Serikali za Mitaa:** Hawa ni mamlaka ya ajira, kuthibitisha kazini na nidhamu kwa watumishi walio chini yao isipokuwa wale wanaoteuliwa na Rais na wale wanaoteuliwa na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

- **Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma:** Mbali na majukumu yaliyotajwa hapa juu, ana madaraka ya kuunda, kusimamia, kutathmini, kuhuisha na kutafsiri Sera za Utawala na Utumishi, kuunda Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma, kusimamia ajira za wageni na kupanga viwango vya mishahara. Huyu ndiye msaidizi mkuu wa Katibu Mkuu Kiongozi katika masuala ya Utawala wa Utumishi wa Umma (Public Service Administration).

- **Idara ya Utumishi wa Walimu (Teachers Service Department) katika Tume ya Utumishi wa Umma:** Ni mamlaka ya usajili wa walimu wote pamoja na mamlaka ya ajira na nidhamu ya walimu wote walio katika utumishi wa umma.

4.0 UTARATIBU WA AJIRA

Katika kutekeleza majukumu yao, Mamlaka za Ajira katika utumishi wa Umma zitatumia Bodi za Ajira kwa upande wa Utumishi wa Serikali za Mitaa na Kamati Maalum za Ajira kwa upande wa Utumishi wa Serikali Kuu, Watumishi wa Afya, Watumishi wa Huduma za Zimamoto na Uokoaji na Uhamiaji na watumishi wa Huduma za kawaida (Operational Service). Aidha kutakuwa na Kamati za Ajira katika Mikoa na Wilaya kwa ajili ya Utumishi wa Walimu. Bodi na Kamati za Ajira ni kama zifuatazo:

(i) Halmashauri za Serikali za Mitaa:

Kutakuwa na Bodi za Ajira katika Halmashauri za Serikali za Mitaa. Bodi hizi zitaundwa na Halmashauri husika na zitakuwa na majukumu ya kusimamia ajira katika Serikali za Mitaa kama ilivyoainishwa katika Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003. Majukumu ya Bodi ni pamoja na kusaili na hatimaye kuwasilisha majina ya waliofaulu usaili kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ataajiri mtumishi/ watumishi miongoni mwa waombaji waliofaulu usaili baada ya kushauriana na Halmashauri husika. Bodi hizi zitakuwa na wajumbe kama ifuatavyo:

- Mwenyekiti -ambaye atateuliwa na Halmashauri husika kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma.
- Mjumbe mmoja - atateuliwa na Halmashauri husika miongoni mwa wajumbe wa Halmashauri hiyo ili mradi asiwe ni Mwenyekiti wa Halmashauri husika.
- Katibu Tawala wa Wilaya au mwakilishi wake.
- Mtaalam anayehusika na masuala ya Serikali za Mitaa katika Sekretarieti ya Mkoa.
- Mwakilishi wa Tume ya Utumishi wa Umma.
- Mkuu wa Idara ya Utawala katika Halmashauri husika atakuwa Katibu na hatakuwa na haki ya kupiga kura.

(ii) Wizara, Idara zinazojitegemea na Mikoa:

Kutakuwa na Kamati Maalum za Ajira ambazo zitawezesha ajira za watumishi wa Umma kufanyika kwa njia ya ushindani katika sehemu hizo kama ilivyoainishwa katika Kanuni Na. 9(3) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003. Kamati hizi zitaundwa na Mamlaka za Ajira yaani **Watendaji Wakuu** katika Wizara, Idara Zinazojitegemea na Mikoa. Majukumu ya Kamati ni pamoja na kusaili na hatimaye kuwasilisha majina ya waliofaulu kwa Mamlaka ya Ajira ambayo itaajiri mtumishi/watumishi miongoni mwa waombaji waliofaulu usaili baada ya kushauriana na kiongozi wa sehemu ya kazi.

Wizarani:

Kamati Maalum za ajira katika Wizara zitakuwa na wajumbe wafuatao:

- Mwenyekiti - atateuliwa na Mtendaji **Mkuu** husika.
- Mjumbe/Katibu - Mkurugenzi wa Idara ya Utumishi na Utawala.
- Wajumbe watatu Watateuliwa na Mtendaji husika.
- Mwakilishi wa Tume ya Utumishi wa Umma.
- Mkuu wa Idara/Kitengo ambayo/ambacho nafasi iliyowazi inatakiwa kujazwa.
- Mjumbe -Afisa Tawalal Utumishi **Mkuu** mmoja kutoka Idara ya Utawala na Utumishi.

Idara zinazojitegemea:

Kamati Maalum za Ajira katika Idara zinazojitegemea ambazo zitakuwa na wajumbe wafuatao:-

- Mwenyekiti - atateuliwa na Mtendaji Mkuu husika;
- Wajumbe wawili - watateuliwa na Mtendaji Mkuu husika:
- Mwakilishi wa Tume ya Utumishi wa Umma:
- Mkuu wa Idara Kitengo ambayo/ambacho nafasi iliyowazi inatakiwa kujazwa.
- Afisa Mfawidhi msimamizi mkuu wa Utumishi na Utawala wa Idara inayojitegemea atakuwa **Katibu.**

Mkoani:

Kamati Maalum za Ajira katika Mikoa zitakuwa na wajumbe wafuatao: -

- Mwenyekiti -atateuliwa na Katibu Tawala wa Mkoa husika
- Wajumbe watatu -watateuliwa na Katibu Tawala wa Mkoa husika
- Mwakilishi wa Tume ya Utumishi wa Umma.
- Afisa anayesimamia Utumishi na Utawala Mkoani ambaye atakuwa Katibu.
- Katibu Tawala wa Wilaya yenye nafasi wazi inayotakiwa kujazwa.

(iii) **Idara ya Utumishi wa Walimu katika Tume ya Utumishi wa Umma** itakuwa na Kamati za Ajira kwa ajili ya Walimu. Kamati hizi zitaundwa na Tume ya Utumishi wa Umma baada ya kushauriana na Waziri anayeshughulikia masuala ya Elimu kwa mujibu wa Kifungucha29 (2)cha Sheriaya Utumishi wa UmmaNa.8 ya mwaka 2002, ikisomwa kwa pamoja na sehemu ya kumi (Part X B) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2003. Kamati husika zitakuwa na Wajumbe wafuatao:

- Kamati za Mikoa
- Mwenyekiti
- Katibu
- Wajumbe watatu

- Kamati za Wilaya

- Mwenyekiti
- Katibu
- Wajumbe watatu

(iv) Vikao vya Bodi na Kamati za ajira:

Bodi na Kamati za ajira zitakutana pale Mamlaka za Ajira zitakapotaka kuajiri watumishi wa Umma au kushughulikia masuala mengine ya kiutumishi.

5.0 MAMLAKA ZA RUFAA:

(i) Kwa Watumishi wa Umma ambao Mamlaka yao ya Nidhamu ni Katibu Mkuu Kiongozi. Mamlaka ya Rufaa ni RAIS.

(ii) Kwa Watumishi wa Umma ambao Mamlaka zao za Nidhamu ni Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Makatibu Wakuu wa Wizara, Wakuu wa Idara za Serikali Zinazojitegemea, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri za Serikali za Mitaa. Mamlaka ya Rufaa ni TUME YA UTUMISHI WA UMMA.

(iii) Kwa Watumishi wa Umma ambao Mamlaka zao za Nidhamu ni Kamishna wa Huduma za Zimamoto na Uokoaji na Mkurugenzi wa Uhamiaji. Mamlaka ya Rufaa ni TUME YA UTUMISHI WA UMMA.

(iv) Kwa watumishi ambao wapo katika kundi la "Operational Service" na Mamlaka yao ya Nidhamu ni Mkuu wa Idara. Rufaa zao zitashughulikiwa kwa mujibu wa Sheria ya Usalama Kazini ya Mwaka 1964 (Sheria N a.16 ya 1964) au sheri a yoyote itakayokuwa inatumika kuhusiana na watumishi hawa.

(v) Kwa Walimu wahopo katika Utumishi wa Umma. Mamlaka ya Rufaa ni TUME YA UTUMISHI WA UMMA. Rufaa za Walimu zitashughulikiwa kwa mujibu wa Kanuni ya 12(ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003.

(vi) RAIS atakuwa Mamlaka ya mwisho ya Rufaa kwa maamuzi yatakayofanywa na Tume.

6.0 MAMLAKA YA ZIADA YA RAIS:

6.1 Inasisitizwa hapa kuwa bado RAIS ni:-

(a) Mamlaka ya kuanzisha na kufuta madaraka ya namna mbalimbali katika Utumishi wa Umma, na

(b) Mamlaka ya kumstaafisha/kumuondoa Kazini kwa Manufaa ya Umma mtumishi katika Utumishi wa Umma.

7.0 SHERIA TANGULIZI ZILIZOFUTWA

7.1 Katika mabadiliko haya, Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya 2002 imezifuta Sheria zifuatazo, pamoja na Kanuni (Regulations) na Taratibu za Uendeshaji wa Utumishi (Service Scheme) zilizotengenezwa kwa muj ibu wa matakwa ya Shena hizi:-

(a) Shena ya Utumishi Serikalini (Civil Service Act), 1989. (b) Shena ya Utumishi wa Serikali za Mitaa (Local Government Service Act) 1982.

(c) Shena ya Tume ya Utumishi wa Walimu (Teachers Service Commission Act) 1989

(d) Sheria ya Utumishi wa Huduma za Zimamoto na Uokoaji (Fire and Rescue Forces Service Act), 1985.

7.2 **Watumishi wa umma ambao hawakujumuishwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma:** Wapo watumishi wa umma walioruhusiwa kuendelea kutumia sheri a na kanuni zao ingawa wanaongozwana Seta yaMenejimenti naAjirakatika Utumishi wa Umma. Watumishi hao ni Askari Polisi na Magereza, Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Bunge na Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Mahakama. Sheria za makundi zitaainishwa ili ziendane na Sera bila kuathiri uhuru na utendaji kazi wa makundi husika.

8.0 WANAOHUSIKA MOJA KWA MOJA NA SHERIA YA UTUMISHI WA UMMA NA. 8 YA 2002 NA KANUNI NA TARATIBU ZAKE ZA UENDESHAJI

Hivyo basi, sasa watumishi wote wa Umma watatumia Sheria inayotawala Utumishi wa Umma na Kanuni zake pamoja na Taratibu za Uendeshaji wa Utumishi wa Umma yaani "PUBLIC SERVICE ACT", 2002, "PUBLIC SERVICE REGULATIONS", 2003 na "PUBLIC SERVICE SCHEME," 2003.

Aidha Taratibu za Uendeshaji wa Utumishi wa Umma (Public Service Scheme) za mwaka 2003 ambazo zimetayarishwa kwa mujibu wa Sheria hii mpya ya Utumishi wa Umma zitakuwa mhimili wa utayarishaji wa Taratibu za Uendeshaji wa Utumishi wa Makundi yote yanayojumuishwa katika Utumishi wa Umma ambazo ni pamoja na Taratibu za Uendeshaji katika Utumishi wa Serikali Kuu (CIVIL SERVICE SCHEME), Utumishi wa Serikali za Mitaa (LOCAL GOVERNMENT SERVICE SCHEME), Utumishi wa Afya (HEALTH SERVICE SCHEME), Utumishi wa Walimu (TEACHERS SERVICE SCHEME), Utumishi wa Huduma zaZimamoto na Uokoaji na Utumishi wa Uhamiaji (FIRE AND RESCUE SERVICE AND IMMIGRATION SERVICE SCHEME). Ili kuharakisha utekelezaji wa sheria hii; Wizara zinazohusika na utarayarishaji wa Taratibu za Uendeshaji Wa Utumishi wa Makundi yote ya Utumishi wa Umma wanatakiwa kutayarisha taratibu hizo katika kipindi kisichozidi miezi mitatu (3) kuanzia tarehe ambayo Waraka huu utaanza kutumika.

9.0 MFUMO WA MAWASILIANO, UWAJIBIKAJI NA UTII.

Mfumo mzima wa mawasiliano, uwajibikaji na utii katika utumishi wa Umma utaendele kuzingatiamtiririko waMamlaka na madaraka katika utumishi wa Umma bila kusahau dhana ya kuaminiana na kuheshimiana (Mutual Trust and Confidence) wakati wote wa kutekeleza majukumu yoyote yanayohusu utawalana utumishi wa Umma.

10.0 Kanuni za Kudumu (Standing Orders), 1994 zinafanyiwa marekebisho ill kukidhi mabadiliko na matakwa ya Sheria Na.8 ya 2002.

11.0 Waraka huu hauna.budi kusomwakwa pamoja na Sera ya Menejimenti yaAjira katika Utumishi wa Umma ya 1999 na unafuta Waraka wa Watumishi wa Serikali Na.1 wa mwaka 1977 na Na.16 wa 1990 na unaanza kutumika tarehe 15 Aprili, 2004.

JOSEPH A. M. RUGUMYAMHETO,
Katibu Mkuu (Utumishi)